

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: +255 26 2322129
Nukushi: 255 26 2322128
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba, Dodoma,
2 Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**KUPOKEA TAARIFA YA KUSIMAMIA HAKIMILIKI NA UGAWAJI WA
MIRAHABA NA MASHUJAA WA JUMUIYA YA MADOLA**

Agosti 11, 2022 – Dodoma

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa kesho Agosti 12, 2022, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kupokea taarifa rasmi ya namna bora ya ya kusimamia HAKIMILIKI na Ugawaji wa Mirahaba kwa wasanii nchini kutoka kwa Kamati aliyoiteua Julai Mosi mwaka huu katika Ukumbi wa Kimataifa ya Mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere kuanzia saa 11 jioni jijini Dar es Salaam.

Uteuzi wa Kamati hiyo, ulitokana na malalamiko ya wadau hususan wa Sekta ya Sanaa nchini kuhusiana na namna mirabaha inavyokusanywa na kugawanywa, kuwepo kwa vitendo vya uharamia katika kazi zao na elimu duni kwa wadau kuhusu masuala hayo.

Aidha, uundaji wa Kamati hiyo ulitokana na maelekezo ya Mhe. Rais ya kuitaka Wizara kusimamia na kutafuta muarobaini wa changamoto za mirabaha kwa wasanii aliyoitoa Mei 30, 2022 jijini Dar es Salaam.

Pia, Mhe. Mchengerwa anatarajia kuwakaribisha nyumbani na kuwapongeza wachezaji mashujaa walioweza kurejea na medali kutoka kwenye Mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyomalizika hivi karibuni Birmingham nchini Uingereza.

A handwritten signature in blue ink that reads "John Mapepele".

John Mapepele

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

